# PENDO LAKO YESU LIMENIVUTIA.

FRT. CANADA
KIPALAPALA:28.5.2004.




2.a). Uliumba kwa pendo lako - nikawepo kwa pendo lako;

b). Waniita kwa pendo lako - naitika pendo lako.

c). Niongoze kwa pendo lako - nijalie hekima yako.

d). Pendo lako ni neno jema - nieneze kwa mataifa.

3. a). Pendo lako mchungaji mwema - nikachunge kundi lako;

b). Pendo lako mwalimu mwema - nifundishe kwa jina lako.

c). Pendo lako kuhani mwema - nitolee dhabihu zako;

d). Pendo lako nabii mwema - nijulishe nyakati zako.

4. a). Pendo lako ni la ajabu - pendo lako zawadi kwangu;

b). Pendo lako ni la ajabu - nitasifu kwa nguvu zangu.

c). Pendo lako ni la ajabu - pendo lako utume wangu;

d). Pendo lako ni la ajabu - nitanena ukuu wako.

**N.B. Unaweza kuweka ala katikati ya ubeti (a,b - ala - c,d) ndipo ala na kurudi kiitikio.**

**Hata hivyo ni chaguo lako kama inaonekana kufaa.**